OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA

SHULE YA SEKONDARI NSEMULWA

S.L.P 556,

MPANDA.

KUMB.NA NSEM/JOINS/2021/2022

SIMU:0755367871/0769013008

MPANDA

JINA LA MWANAFUNZI

……………………………………………………………………………………..……

S.L.P. ………………………………….

MPANDA.

**Kuh:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NSEMULWA 2022.**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022 katika shule ya sekondari Nsemulwa.Ushirikiano wako pamoja na wanafunzi wenzako ni siri kubwa ya mafanikio yako.Hii inawezekana ukiwa na NIDHAMU,JUHUDI NA MAARIFA.Ukiwa hapa shuleni utakuwa na wajibu mkubwa wa kusoma kwa bidii,kufuata sheria za shule,kushiriki katika mipango ya elimu ya kujitegemea na shughuli zingine zozote zitakazopangwa pamoja na kufuata taratibu zote za shule zitakazotolewa na viongozi wako shuleni. HILI NDILO LIWE LENGO LAKO UTAKAPOKUWA SHULENI.

Shule itafunguliwa tarehe **10/01/2022** muda wa saa **1:30 asubuhi**.Tafadhari ripoti mapema tayari kwa kuanza masomo. Kinyume na hapo nafasi yako itachukuliwa na mtu mwingine.

i. SARE YA SHULE

**WAVULANA**

- Suruali mbili (02)bluu bahari zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh14,000/=kwa kila moja.
- Mashati mawili(02) meupe mikono mifupi
- Viatu vyeusi jozi mbili(02) vya kamba na vyenye kisigino kifupi.
- Soksi nyeupe jozi mbili(02) fupi.
- Mkanda mweusi wa ngozi usio na marembo.
- Mkoba mweusi wa kubebea madaftari
- **T-sheti (01) yenye kola nyeupe (maarufu kama form six) rangi ya bluu nyeusi (dark blue) yenye nembo ya shule, ITAPATIKANA SHULENI KWA ELFU KUMI NA TATU TU. (Tsh. 13000) na itavaliwa siku ya Ijumaa ikiwa ni sehemu ya sare ya shule.**

**WASICHANA**

- Sketi za malinda rangi ya bluu bahari, malinda yenye upana wa cm .05. Belt upana wa cm 07. **Sketi nazo zitapatikana shuleni kwa gharama ya tsh. 14000.**
- Blauzi nyeupe(02) za mikono mifupi
- Viatu vyeusi vya mkanda mmoja vya rangi nyeusi na vyenye kisigino kifupi.
- Mkoba mweusi wa kubebea madaftari
- Kama ni binti wa Kiislam ashone hijabu nyeupe.
  **NB: Kitambaa kiwe cha suti.**

  **T-sheti (1) yenye kola nyeupe (maarufu kama form six) rangi ya bluu nyeusi (dark blue) yenye nembo ya shule ITAPATIKANA SHULENI KWA ELFU KUMI NA TATU TU(Tsh 13,000/=) na itavaliwa siku ya Ijumaa ikiwa ni sehemu ya sare ya shule.**

ii. VIFAA VYA DARASANI

- Daftari kubwa kumi na moja (11) ambazo ni aina ya counter book kuanzia **Quire two** na kuendelea.
- Kalamu na mkebe wa hesabu (mathematical set)
- Kamusi moja(dictionary)

**NB: Serikali inatoa huduma za karatasi ambazo hazitoshi kufanya mitihani ya mara kwa mara kwa kila wiki,mwezi na mihula yote Hivyo kila mwanafunzi aje na bunda moja la karatasi A4(rimu)kwa mwaka kwa ajili ya kuongeza kufanya mitihani husika kwa mwanafunzi husika na sio pesa tasilimu.**

iii. CHAKULA

Suala hili litapangwa na wazazi katika kikao cha wazazi mara tu baada ya kufungua shule.

iv. VIFAA VYA MAZINGIRA

- WASICHANA:Walete ndoo moja ya lita kumi na kwanja la kufyekea lililo nolewa.
- WAVULANA:Walete jembe lenye mpini pamoja na fagio.

**MAHALI ILIPO SHULE YA SEKONDARI NSEMULWA.**

**Shule ya Sekondari Nsemulwa ipo Mtaa wa Airtel, kata ya Uwanja wa Ndege, Barabara ya kwenda Tabora**.

v. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a. Wizi
b. Uasherati
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli n.k.
e. Kupigana au kupiga.
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g. Kudharau Bendera ya Taifa.
h. Kuwa mjamzito/kupata mimba.
i. Kutoa mimba.
j. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
k. Kukataa adhabu kwa makusudi.
l. Kuwa na simu ya mkononi.

**TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI**

Shule inapenda kupata taarifa muhimu za kila mwanafunzi kwa ajili ya mawasiliano wakati wowote awapo shuleni.Fomu hii ijazwe kwa usahihi na ukamilifu.

Jina la mwanafunzi………………………….kidato……………….mwaka……/……/……..

Anwani ya nyumbani(anayotumia)…………………Tarehe ya kuzaliwa……/……/……..

Namba ya simu ya (nyumba/mzazi)………………Mtaa/kijiji anachotoka……………

Kata…………………..Tarafa…………………..Wilaya………………Mkoa…………………

Shule ya msingi aliyosoma……………………………Dini yake ni……………………

(mkristo,mwislamu n.k) Dhehebu lake ni ……………………..Mkatoliki,Mlutheri,Suni n.k)

Sahihi…………………………Tarehe.…./……/……

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi…………………………………………………………………..NAKUBALI/SIKUBALI nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Nsemulwa.Naahidi kuwa nitazitii taratibu,kanuni na sheria zote za shule.Nitafuata masharti yote yanayo tolewa na mkuu wa shule,na wafanyakazi wote na viongozi wote wa shule.Ninaahidi pia nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo,kazi za nje na katika michezo kwa muda wote nitakaokaa Nsemulwa Sekondari.Nakiri kuwa kwa akili zangu timamu,taarifa zote nilizotoa hapo juu ni sahihi zinanihusu.

Jina……………………………..…Sahihi……………..Tarehe………./……..../…………

TAARIFA YA MZAZI/MLEZI

Jina la mzazi/Mlezi……………………………………….

Anwani yake………………………………………………

Namba ya simu……………………………………………

Kazi anayofanya………………………………………….

Wilaya/Mji anakofanyia kazi……………………………..

Anwani ya kazini………………………………………….

Namba ya simu ya kazini…………………………………

AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi…………………………………MZAZI/MLEZI NAKUBALI/SIKUBALI nafasi aliyopewa mwanangu katika shule ya sekondari Nsemulwa.Naahidi kuwa nitawajibika /Sitawajibika na kumhimiza mwanangu kuzitii taratibu,kanuni na wafanyakazi wote wa shule.Ninaahidi pia nitashirikiana/Sitashirikiana na uongozi wa shule kumhimiza mwanangu kushirikiana na wanafunzi wenzake katika shughuli za masomo ,kazi za nje na katika michezo na kuwa na nidhamu kwa muda wote atakao kaa Nsemulwa Sekondari.Nitapenda/Sitapenda kupata taarifa zote zinazomhusu mwanangu muda wote awapo shuleni (futa isiyo husika)

Jina…………………………………….……Sahihi………………..Tarehe……/……./……..

vi. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria namba 25 mwaka 1978 na kama ilivyoboreshwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

- Mwanafunzi anapaswa kuwepo eneo la shule wakati wote isipokuwa anapopata ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu ,Makamu mkuu wa shule au mkuu wa shule.
- Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare rasmi ya shule muda wote wa shule (Darasani)isipokuwa muda wa kazi za mikono na michezo ambapo atavaa nguo rasmi za kazi/michezo.
- Lugha chafu matusi,ugomvi,fitina na kupigana kwa mwanafunzi ni mwiko kabisa.
- Mwanafunzi lazima awahi popote anapotakiwa na wakati uliowekwa.
- Mwanafunzi ni lazima aiheshimu kazi ya darasani na nje na kuifanya vizuri.Ni lazima kufanya mazoezi ya mitihani yote inayotolewa awapo shuleni.
- Unywaji wa vileo,kuuza pombe na uvutaji wa aina yoyote ya sigara au madawa ya kulevya ni mwiko kwa mwanafunzi.Hairuhusiwi kufanya biashara yoyote shuleni.
- Wizi wa aina yoyote ni marufuku na ni kosa kubwa kwa mwanafunzi.
- Uharibifu na upotevu wa mali binafsi au ya umma pia ni kosa kubwa.
- Mwanafunzi anapaswa kuwa na heshima, utiifu na mwenye adabu wakati wote na kwa kila mtu. Ukaidi na ubishi kwa viongozi wake ni marufuku.
- Wageni wa mwanafunzi wanaruhusiwa kuonana na mwanafunzi baada ya kujitambulisha na kupokelewa na mwalimu wa zamu. Wanafunzi watembelewe muda wa mapumnziko.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuoa / kuolewa wakati bado akiwa shule. Akibainika atafukuzwa shule mara moja. Aidha ni marufukuku kuwa na mahusiano ya kimapenzi awapo shuleni au nyumbani kipindi chote cha uanafunzi wake. Akibainika atafukuzwa shule mara moja.
- Ni mwiko kwa mwanafunzi kwenda kwenye nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu bila ruhusa au kibali maalumu toka kwa mwalimu mlezi au uongozi wa shule.
- Mapambo na nakshi za aina yoyote na mavazi ya kihuni kwa mwanafunzi ni marufuku, nywele ziwe fupi, ndevu ni marufuku. Mitindo ya kunyoa kama pank, kunyoa kipara pasipo sababu za msingi hatutavumilia na adhabu kali itatolewa kwa atakayefanya kinyume na haya (Aidha kofia aina yoyote, mikanda mipana na majaketi marufuku kabisa shuleni). **Simu haziruhusiwi ukikamatwa utapewa adhabu kali ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule na simu yako itaharibiwa kabisa.**
- Kukataa adhabu ni kukataa malezi bora ya walezi wako shuleni yenye maana ya kukataa kuwa mwanafunzi wa shule hii.
- Mgomo wa aina yoyote ni marufuku na ni haramu katika Tanzania. Matatizo yote yatashughurikiwa kwa kufuata ngazi zilizowekwa tangu darasani hadi baraza la shule. Atakayegoma au kusababisha mgomo adhabu yake ni **kufukuzwa shule.**

**…………………………..**

**JACKSON E. MJWANGA**

**MKUU WA SHULE**

FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA / WILAYA NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI NA KUIKABIDHI KWA MKUU WA SHULE.

Mimi ( Jina la mganga mkuu wa Mkoa / Wilaya)………………………………………..

Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la Mwanafunzi)……………………………

Amepimwa na mimi kikamilifu na kuonesha kuwa anayo / hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo:

**A) Hali ya mwili**

- Mapigo ya moyo……………………………………………
- Haemoglobin……………………………………………..
- Kundi la damu (Blood group) ……………………………………………………..
- Mkojo………………………………………..
- Haja kubwa……………………………………
- Macho yana kasoro………………………………………………..
- Masikio yana kasoro…………………………………………………

  NB: Weka maoni yako kuhusu kile kilichotajwa…………..................................
  ……………………………………………………………………………………
  ……………………………………………………………………………………
  …………

**B) Magonjwa**

Amewahi / hajawahi au hana magonjwa yafuatayo:

- Tuberculosis…………………………………………
- Epilepsy……………………………………..
- Blood pressure………………………………………….
- Peptic diseases……………………………………………
- Sickle cells……………………………………………….
- Ukoma……………………………………………..
- Venereal diseases (Give type) …………………………………………………
- Mental illiness……………………………………………..
- Any other serious disease not mentioned above………………………
  ……………………………………………………………………………
  ……………………………………………………………………………
  ……………………………………………………………………………
  - ➢ Coments from the Doctor in charge…………………………
    ……………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………
    …………

    Sahihi na muhuri wa Daktari / Mganga wa Hospitali ya Serikali.

………………………

…………………………………